


# Muda Zaidi pamoja na Max



**Na Ashlyn B., umri miaka 12,  
Washington, Marekani**

Siku moja nilienda kukita kambi ufukweni pamoja na familia yangu, marafiki wachache na mbwa wangu Max. Tuliogelea na kucheza siku nzima. Kisha tukatazama baruti wakati giza lilipoinga. Sote tulikuwa na wakati mzuri sana.

Baruti zilipoisha, nilimtafuta Max. Lakini alikuwa hayupo! Niliingwa wasiwasi na kupiga yowe kwamba Max amepotea. Machozi yalipokuwa yakinitiririka usoni, sote tulimtafuta msituni. Nilihisi sauti ndogo ikiniambia nisali, kwa hiyo nilifanya hivyo. Lakini mwili wangu wote ulihisi kunyong'onyea kama tamba na nilimhofia Max.

Hatukumpata, kwa hiyo tulirejea hadi kwenye hema letu. Niliendelea kusali kichwani mwangu, lakini nilianza kupoteza tumaini.

Nililia mpaka nikalala.

Masaa machache baadaye, wazazi wangu waliniamsha. Max

alikuwa ameketi kando yangu! Wazazi walisikia sauti ya mlio wa njuga wa mkanda wa Max nje ya hema letu. Nilimkumbatia sana na kimya kimya nikamshukuru Mungu kwa kujibu sala zangu.

Miaka mitatu baadaye, Max aliumiza mgongo wake na alikuwa na maumivu makali sana. Hakuweza kupona, kwa hiyo ilibidi tuachane naye. Baba wa Mbinguni alinifariji na kunipa amani. Roho Mtakatifu alinikumbusha kwamba tungempoteza Max miaka mitatu iliyopita, lakini Mungu alitusaidia tumpate. Nina shukrani kwamba Yeye alitupatia muda zaidi wa kumpenda Max.

Ninajua Mungu hujibu sala na kutoa faraja katika majaribu. Upatanisho wa Yesu Kristo ni kwa ajili ya kila mtu. Ninashukuru sana kwa ajili ya kile ambacho Yesu Kristo na Baba wa Mbinguni wamenifanyia mimi na familia yangu. ●

